GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZUU NO. **251** Dhl/Qadah-Hijjah **1446** AH Mei– **2025** Hijrat **1404** HS BEI TSH 800/=

WAJIBU WA MWAHMADIYYA KWA UKHALIFA

Sheikh Shahab Ahmad, Mtwara


UK. 03

Kila mwaka, tarehe 26 ya mwezi wa Mei inatukumbusha Ukhalifa ulianzishwa ndani ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Hii ni siku ya kukumbuka neema moja kubwa ya Mwenyezi Mungu na kutoa shukrani yake ambayo Waislamu wengi bado wanaitamani. Pia, ni siku ya kukumbushana nini kinachotakiwa kufanyika ili sisi tudumu kupata baraka za Ukhalifa.

Hazrat Amirul Muminin Khalifatul Masihi wa Tano (atba) katika hotuba zake mbalimbali aliwahi kueleza mwahmadiyya ana wajibu gani kwa Ukhalifa. Alisema:

"Kama mnapenda kupata maendeleo na kushinda dunia nzima nasaha zangu ni hizi na ujumbe wangu ni huu kwamba shikamaneni na ukhalifa, shikeni kwa nguvu kamba hii ya Allah, kwani leo maendeleo yetu yote yanategemea ukhalifa."

(AlFazl International, 23-30 Mei 2003)

Kisha alisema:

JUHUDI NA VIKWAZO KATIKA KUIPATA AMANI YA CONGO DRC.

Na. Rajabu Mkieti


UK. 04

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ni moja kati ya Taifa kubwa sana barani Afrika , ni nchi yenye eneo la mita za mraba zaidi ya 2,344,858 sawa na Maili mraba 905,355 iliyoko kusini mwa Jangwa la Sahara.Taifa hili, limebarikiwa maliasili za aina mbalimbali , ikiwamo madini ya shaba; uwezo wa uzalishaji umeme wa maji, ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo na msitu wa pili kwa ukubwa duniani.Lakini kwa bahati mbaya, watu wake wengi, hawajanufaika na urithi wa utajiri rasilimali hizo. Nchi ya Kongo

MAJIBU YA BAADHI ZA SHUTUMA/PINGAMIZI DHIDI YA SEYYIDNA AHMAD[AS] KUWA KWAKE IBN MARYAM UK. 04

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

NDUMILA KUWILI SI MWEMA

Ni lini na wapi uliwahi kusikia watu wakakaa kitako na kupanga kuanzisha kwa taifa? Wapi ulisikia habari hii? Na ikapangwa kwamba hao wenyeji, mwenye mali, wenye chao kwa miaka twende miaka rudi wawekwe pembeni? Wapi ulikaa na kusikia watu wazima na akili zao kichwani wakikaa na kupendekeza taifa hilo la wateule litakuwa kama ikiwezekana Uganda, Kenya, Argentina.

Kukaa chini na kufikiria kutengeneza taifa ni kioja katika historia. Lini ulisikia mashirika yanaanzishwa, yanakusanya pesa, wananunua ardhi taratibu, baadae wanahamia na kuanzisha ubaguzi wa rangi? Ardhi yote inachukuliwa na wenyeji mnakuwa wageni. Ni kwa vipi taifa linalojigamba linaloelewa utawala wa sharia na haki za binadamu linakumbatia 'Mashylock' kuwa wewe nenda kinyume na Ujerumani na Uturuki na mambo haya yakishatulia tutawapatia uhuru, kana kwamba uhuru ni zawadi na sio haki ya binadamu.

Nadhani hujawahi kusikia watu wazima kimwili na sio kiakili wakivunja ahadi walizozitoa. Ana thamani gani mtu anayevunja ahadi? Bila shaka huna habari ya watu hao waliopewa ahadi ya uhuru, basi elewa kuwa wapo. Hata bila kuulizia, wakaona walowezi wakiingia kwa wingi na kuanza kuwagombanisha, sera yao ya siku nyingi; 'wagawe uwatawale'.

Aliyekuwa pale ananyanyaswa na kuwa raia daraja la pili. Mauaji kila pembe kutoka kwa watawala na walowezi. Umewahi kuona aliyepora shamba akiona hilo halitoshi na kwa sababu ya mjomba mwenye nguvu wakakuchangia na kukunyang'anya ardhi yako yote. Ardhi yote sasa imejaa vifusi. Mjomba nae akanogewa na kuleta mitaji yake. Atatoka hapo penye minofu?

Tangu umezaliwa ni lini uliposikia sheria zote za kimataifa kuhusu vita na haki za binadamu zikisagwa tikitiki kwa kiburi na majivuno?

Ukimuona tembo yuko juu ya mti, kuna aliyempandisha. Na hivyo huyo huyo ndiye atakayemteremsha.

Lakini kabla tembo huyo hajateremshwa huku hata maneno ya kueleza hali ilivyo hayapatikani, watoto wanauawa usiku na mchana, hospitali zimefurika hazina umeme wala maji, hakuna chakula, tunajiuliza kizazi kijacho kitakapokuja kuelezwa yanayoendelea kitashindwa kuelewa hivi kweli walikuwepo binadamu waliokaa kimya na kutizama watoto wakiuawa kama nzige, binadamu akiambiwa toka hapa asubuhi na jioni anaambiwa nenda kule. Hospitali zikiteketezwa, watoto na vibakuli mkononi wakigombea chakula, waandishi wa habari wakiuawa kwa wingi kuliko vita yoyote ya hivi karibuni. Tunatizama. Historia itatuuliza. Na sijui jibu tutalipata kutoka wapi.



QUR'AN TUKUFU

"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao na kwa yakini atawaimarishia dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia Amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na cho chote. Na atakaye kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri."

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ
لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِى الْاَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِيْنَ مِنْ
قَبْلِهِمْ ۪ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِيْنَهُمُ الَّذِى ارْتَضٰى لَهُمْ
وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِّنْۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ اَمْنًا ؕ يَعْبُدُوْنَنِىْ
لَا يُشْرِكُوْنَ بِىْ شَيْـًٔا ؕ وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ
هُمُ الْفٰسِقُوْنَ ۝



NUKUU YA HADITHI

Imesimuliwa na Hadhrat Hudhaifa r.a ya kwamba Mjumbe wa Allah[saw] alisema: Unabii utakuwa baina yenu Apendapo Allah. Kisha Atauondoa. Kisha utakuwapo ukhalifa juu ya njia ya unabii Allah Atakapopenda uwepo, Kisha Atauondoa pia. Kisha utapatikana ufalme wa kuudhi ambao utakuwa mpaka Allah apendapo kuwepo, kisha Allah Atauondoa Kisha utapatikana ufalme wa mabavu na utaendelea hadi Allah akipenda uwepo, kisha Atauondoa. Kisha utapatikana ukhalifa juu ya njia ya unabii. Kisha (Mtume s.a.w) akanyamaza.
(Musnad Ahmad bin Hanbal).



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

"Basi, enyi wapenzi, kwa kuwa hii ndio sunna ya Allah tangu kale ya kwamba Mwenyezi Mungu huonyesha kudra mbili ili kuzikanyagalia mbali furaha mbili za bandia za wapinzani, hivyo haiwezekani sasa ya kuwa Mwenyezi Mungu aziache sunna zake za zamani. Kwa hiyo msihuzunike kwa habari niliyowaambieni wala nyoyo zenu zisifadhaike, kwani hamna budi kuiona kudra ya pili vilevile. Na kuja kwake ni bora kwenu kwa sababu hiyo itadumu, nayo itaendelea bila kukoma mpaka kiyama. Na hiyo kudra ya pili haiwezi kuja mpaka niondoke. Lakin niondokapo, hapo Mungu atakutumieni hiyo kudra ya pili itakayodumu pamoja nanyi milele kama Mungu Alivyoahidi katika Barahin-i Ahmadiyya. Ahadi hiyo hainiuhusu mimi bali yawahusuni ninyi, kama alivyosema kwamba nitaishindisha jumuiya hii inayokufuata juu ya wengine hadi kiyama. Basi hapana budi mfikiwe na siku ya mimi kuagana nanyi ili baadaye iwadie ile siku iliyo siku ya ahadi ya kudumu. Mungu huyu ndiye Mungu atimizaye ahadi, Mwaminifu na Mkweli. Ataonyesheni yote Aliyoahidi. ijapokuwa hizi ni siku za mwisho za dunia na ndiyo zama za balaa nyingi kushuka, lakini hapana budi dunia hii ibaki mpaka yote hayo yatimie aliyoniambia Mungu. Mimi nimedhihiri nikiwa kudra moja kutoka kwa mungu. Nami ndimi kudra hasa ya Mungu na baada yangu watakuwapo wengine watakaokuwa onyesho la kudra ya pili. Hivyo basi, endeleeni kuomba mkiwa pamoja ili kuingoja kudra ya pili ya Mungu. (Al-Wasia uk.8-9)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi:	Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri:	Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta:	Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji:	Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji:	Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:	1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga 2. Mahmood Hamsin Mubiru. 3. Sheikh Shahab Ahmad. 4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

WAJIBU WA MWAHMADIYYA KWA UKHALIFA

Kutoka uk. 01



"Kwa fadhila Zake pekee Mwenyezi Mungu Alibadilisha hofu ya wanajumuiya wa Masihi aliyeahidiwa (as) kuwa amani baada ya kufariki kwake, na Jumuiya yake Akaijalia uimara sawa na ahadi zake yaani Aliendeleza nguvu na uimara iliyokuwa nayo na Akathibitisha kwa ushuhuda wake wa kivitendo kwamba yule aliyeahidiwa alikuwa ni mtume na nabii wa Allah. Na alikuwa Khalifa wa Mwenyezi Mungu ambaye katika karne ya 14 alitabiriwa kustawisha tena sheria iliyoshuka kwa Mtume Mtukufu[saw] na kisha baada yake kwa mujibu wa utabiri wa Mtume Muhammad (saw) ukaja ukhalifa wake ambao utaendelea hadi siku ya kiyama. ...

Kila mwanajumuiya mtoto kwa mkubwa, mwanamume kwa mwanamke hushuhudia kwamba yeye alishawahi kuona na anaendelea kuona ushuhuda wa kivitendo wa Allah subhana wa taala. Si wanajumuiya peke yao bali hata wasiokuwa wanajumuiya nao pia wanakubali jambo hili. Mifano iliyotangulia ni mingi sana, baada ya kifo cha Hazrat Masihi aliyeahidiwa (as) kisha baada ya kifo cha Hazrat Khalifa wa kwanza (ra); halafu baada ya kifo cha Hazrat Khalifa wa pili mwana aliyeahidiwa (ra), ... Lakini baada ya kutazama uchaguzi wa Khalifa wa tano uliorushwa kupitia MTA, hata wapinzani walikubali kwamba hatujui ninyi ni wakweli au la hata hivyo inaonekana kwamba ushuhuda wa kivitendo wa Allah subhanahu wa ta'ala uko pamoja nanyi. Ndio maana hii ni fadhila kuu ya Allah subhana wataala juu ya jumuiya ya Ahmadiyya na neema yake ambayo inatakiwa kutolewa shukrani nyingi sana. Na kutoa shukrani kutaongeza neema hii zaidi."
(Khutbat e Masroor, juz. 3 Kur. 307-308)

Kisha alisema:
"Hii ni imani yetu kwamba Mwenyezi Mungu mwenyewe Anamteua Khalifa na hakuna upungufu katika uchaguzi wake. Mwenyezi Mungu Atakayemvisha kanzu hii hakuna yeyote anayeweza kuivuaaukuinyang'anya.Mwenyezi Mungu huwa anamchagua mja wake mdhaifu humuinua na kumpakata na kumsaidia katika kila hali na huzalisha upendo wa Jamaat moyoni mwake kiasi kwamba anaanza kuhisi uchungu wa Jamaat kuwa ni uchungu wake, na hivyo kila mwanajumuiya anafikiria kuwa mtu mmoja mwenye huruma yupo ambaye anajua uchungu wake na kumwombea dua kwa Mwenyezi Mungu. "
(AlFazl, 30 Mei 2003)

Kisha alisema:
"Kwa sasa Allah subhanahu wata'ala Alimteua mtu huyu kuwa Khalifa ambaye machoni pa dunia huenda watu wasimtazamie kuwa chochote wala wasijali hata kumwona, lakini Mwenyezi Mungu haihitaji dunia. ... Mimi nikijiangalia mwenyewe na nikiona udhaifu wangu, Mungu wangu Ananijua zaidi kuliko mimi kwamba kuna sifa gani ndani yangu, hapo ndipo ninakumbuka kudra ya Mwenyezi Mungu. ... Ukhalifa hutokana na Allah subhanahu wata'ala na utaendelea mpaka Atakapopenda Yeye. ... Kumbukeni kuwa huyu ni Mungu mwenye ahadi za kweli. Naye Anaendelea kuitunza Jumuiya nzuri ya Masihi wake mpendwa, Yeye hatuachi asilani abadani, Anaendelea kutimiza ahadi zake Alizofanya kwa Masihi wake jinsi Alivyoendelea katika wakati wa makhalifa waliotangulia. Anaendelea kutujalia rehema na fadhila zake vilevile kama Alivyojaalia huko nyuma; na inshAllah Ataendelea kutujalia. Hivyo jambo hili linatakiwa kuzingatiwa kwamba mtu yeyote asijikwae na asiharibu akhera yake kwa kutokutekeleza mafundisho ya Allah Subhanahu wataala. Kwa hiyo ukishikamana na kishikio hiki imara kwa kufanya dua basi hakuna atakayeweza kukudhuru hata kidogo. Allah Subhanahu wataala Awawezeshe wote kufanya hivyo. Aamin"
(Khutbat e Masroor, juz. 2, Kur. 351-354)

Kisha akituelekeza kuhusu majukumu yetu alisema:

"Kila mmoja wenu ana wajibu wa kudumu kufanya maombi na Ashikamane na ukhalifa na daima akumbuke jambo hili kwamba maendeleo yake yote na mafanikio yake yote yanategemea kuungana na ukhalifa tu. Mtu yule tu anaweza kufaa jumuiya hii anayejiunganisha na imamu, ikiwa yeyote hajiunganishi na imamu hana nafasi yoyote hata kama awe anajua elimu zote za dunia nzima. Maadamu akili zenu na mipango yenu itabaki kuwa chini ya ukhalifa na mtaendelea kutii mwongozo wa imamu barabara, msaada maalumu wa Allah subhanahu wa ta'ala utapatikana kwa ajili yenu."
(AlFazl 30 Mei 2003)

Kisha aliwasihi wanajumuiya akisema:
"Leo dunia imezama katika upuuzi na hakuna anayewaongoza. Jumuiya ya Masihi aliyeahidiwa (as) ni jumuiya pekee inayojiletea mabadiliko mema ya kiroho chini ya bendera ya ukhalifa. Kwa hakika hii ni neema ambayo hatuwezi kutimiza haki ya shukrani yake, lakini Allah Alisema ikiwa mtaendelea kutoa shukrani, si kwa maneno tu bali hata kwa kurekebisha vitendo vyenu, basi Mimi nitaendelea kuwapeni neema zangu. Hivyo (enyi wanajumuiya) endeleeni kufanya dua kwa ajili yake. Ninyi mwaendelee kufanya dua kwa ajili yangu na mimi nifanye dua kwa ajili yenu ili hisia hizi za shukrani na neema za Allah subhana wataala zisikatike kamwe na ziendelee kuongezeka kila wakati."
(Hotuba ya Ijumaa, 30 Mei 2008)

Kisha alisema:
"Ikiwa watu wote wakiendelea kufanya dua kwa ajili ya Ukhalifa na kwa ajili ya Khalifa wa zama; basi jambo hili litavuta fadhila zisizohesabika za Allah subhanahu wataala; kwani dua za wote, imamu na wanajumuiya, zitakuwa na mwelekeo mmoja na zikimwomba Allah neema zake, hapo wanajumuiya watazingatia kuwa kama sisi tunafanya dua basi vitendo vyetu vinatakiwa kuwa sawa na maamrisho ya Mwenyezi Mungu nasi tuelekee pale ambapo Khalifa wa zama anavyotuelekeza kwa mujibu wa mafundisho ya Allah na Mtume wake (saw). Ikiwa watafanya dua kwa hisia hizi basi watapata nafasi ya kujirekibisha na kazi ya imamu ya kuwasimamia itakuwa rahisi. Hivyo, kila mwanajumuiya anatakiwa kuelewa jambo hili kuwa pale imamu anatakiwa kuwa mwadilifu na afanye malezi ya wanajumuiya kwa mujibu wa maamrisho ya Allah na mtume wake, afanye juhudi za kuondoa shida zao na awafanyie dua; vilevile wanajumuiya wanapaswa kujenga dhana hii kuwa kama sisi tunapenda ukhalifa basi tujichunguze hali zetu na kwa kuziingatia hili tuelekeze maisha yetu kwa njia ambayo maisha yetu yanatakiwa kuikanyaga sawa na mafundisho ya Mwenyezi Mungu na mtume wake au kwa njia ambayo Khalifa wa zama anatupenda kuikanyaga."

Mwenyezi Mungu Atupatie uwezo wa kupokea baraka za Ukhalifa kwa kutekeleza wajibu wetu. Aamin

TANGAZO

UONGOZI WA LAJNA IMAILLAH TANZANIA UNAWATANGAZIA LAJNA NA NASRAT WOTE NCHINI KUWA IJTIMAI YA LAJNA IMAILLAH YA MWAKA 2025 ITAFANYIKA TAREHE 20,21 & 22 YA MWEZI JUNI KATIKA ENEO LETU LA KITONGA JIJINI DAR ES SALAAM.

KILA MWANATANZIMU ANAHIMIZWA KUMALIZA MCHANGO WAKE WA IJTMAI NA KUWEKA NIA YA DHATI YA KUHUDHURIA IJTMAI HIYO PAMOJA NA KUJIANDAA KUSHIRIKI KATIKA MASHINDANO YA KIELIMU NA MICHEZO.

PIA WAJUMBE WOTE WA SHURA KUTOKA MATAWI MBALIMBALI NCHINI WANAKUMBUSHWA KUJIANDAA NA SHURA YA KITAIFA ITAKAYOFANYIKA SIKU YA JUMAPILI YA MWEZI JUNI.

WASALAAM.

JUHUDI NA VIKWAZO KATIKA KUIPATA AMANI YA CONGO DRC.

Kutoka Uk 01..



inakadiriwa kuwa na watu zaidi ya Milioni 100 Historia ya DRC ni yakipee sana kwani tofauti na makoloni ya nchi nyingine za Afrika utawala wa koloni la mfalme wa Ubelgiji Leopoid II ulikua ni wa kichekesho sana aliitwa ardhi ya Congo na kuwa milki yake binafsi mnamo February 5, 1885 jambo ambalo limeifanya nchi hiyo kuwa na athari kubwa katika utawala wake hata baada ya ukoloni kuondoka. Historia ya DRC haiwezi katu kuiweka kando dosara ya mwanzo ilitokana na kubeza juhudi za Patrice Lumumba aliyezaliwa July 2,1925 ambaye alipata heshima kubwa katika nchi ya DRC, alikuwa waziri mkuu wa kwanza wa DRC baada ya uhuru Patrice Lumumba alibaini changamoto kadhaa katika Taifa lake utawala wake ukaandaa namna bora ya kuongoza nchi yake aliona njia rahisi ili nchi itawalike kuwe na mfumo wa utawala utakao waunganisha wa Congo hatua hii ilipingwa vikali mno na masalia ya vibaraka wa Ubelgiji kwani ilikutana na upinzani mkubwa sana ajabu ilioje waliona anataka kuanzisha aina ya ufalme wake. Mabeberu wa kibeligiji hawakufurahishwa na juhudi hizo za Patrice Lumumba kwa namna ya ajabu siku chache baada ya uhuru jimbo la Katanga (Jimbo lenye madini mengi sana) likajikuta katika hatua ya kutaka kujitenga huu ulikua mkakati maalumu uliondeshwa chini ya udhamini wakoloni wa Kibelgiji Patrice Lumumba hakupendezwa na hali hii akaingia kazini kuhakikisha anasimamisha vuguvugu hilo ovu juu ya utawala wake matokeo yake alijikuta akiogelea katika mtutu wa bunduki na kupoteza maisha wahaini hao hawakuridhika bado walizidi katika uovu wakaukatakata mwili wake vipande vipande na kuuyesyusha katika asidi na hatimaye ikawa mwisho wa shujaa huyu wa Afrika na Adui machoni mwa wakoloni wa Ubelgiji, ni aibu waliojiona wastaarabu walisimamia kuzika juhudi za kuipata DRC yenye maendelo na neema na kuzaa mgogoro mpya katika Taifa lilitoka kuzaliwa muda mfupi tu. Baada ya kuuwawa kwa Patrice Lumumba Nchi ya DRC iliwekwa mikononi mwa Joseph Mobutu kwa msaada wa wanajeshi Mwaka 1965 Mobutu alichukua madaraka, na baadaye kuibadili jina nchi hiyo na kuiita Zaire na yeye kujiita Mobutu Sese Seko. Katika utawala wake yeye aliangalia sana eno la upande wa Magharibi na kuliweka kando eneo la mashariki ambalo hivi sasa ndio kidonda kinachoitesa amani ya DR Congo utawala wake nao ulikubwa na shutuma nyingi za ufisadi,rushwa na matumizi mabaya ya madaraka baada ya vita baridi, Zaire ilijikuta katikati ya mgogoro mpya hiyo ulikua mwaka 1997, wakati nchi jirani ya Rwanda ilipovamia Zaire kuwasaka wanamgambo wa Kihutu, iliwapa nafasi waasi wanaompinga Mobutu ambao mara moja waliuteka mji wa Kinshasa na Laurent Kabila kuingia madarakani na kuwa Raisi wa Taifa hilo Raisi Laurent Kabila yeye alianza na kazi ya kulirejesha jina lao pendwa la nchi yake Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo DRC. Pamoja na yote aliyoyafanya Raisi Kabila matatizo ya DRC yaliendelea. Mzozo kati ya Bwana Kabila na washirika wake wa zamani ulianzisha uasi mwingine, uliokuwa ukiungwa mkono na Rwanda na Uganda. Angola, Namibia na Zimbabwe zikachukua upande wa Kabila na hivyo kuigeuza nchi hiyo kuwa uwanja wa vita. Juhudi za Raisi Laurent Kabila kuiongoza DRC hazikufua dafu wahasimu wake wakafaulu katika njama zao ovu kwa kukatika uhai wake 2001 Raisi Kabila alipigwa risasi na mlinzi wake wa karibu huu ukawa mwanzo mpya kwa Bwna Joseph Kabila mwanae Bwana Laurent Kabila kuchukua madaraka baada ya kifo cha baba yake yeye aliitawala DR Congo kwa miaka 18 kabla ya Bw Tshisekedi kushinda uchaguzi mnamo Desemba 2018. Wakati wa utawala Joseph Kabila angalau mwanga wa matumaini ya kupata amani ya DRC ulianza kuonekana lakini na yeye alikumbana na vikwazo vyingi haza vita katika eneo hili la masharika vikundi vya uporaji wa rasilimali za nchi vilipungua kwa kiasi na mazungumzo ya amani kwa upande wa maziwa makuu yalishika hatamu ushawishi wa Raisi Joseph Kabila kwa nchi zinazoizunguka Jamuhuri ya DRC ulikua mkubwa na hapo UN umoja wa Mataifa uliona ipo haja ya kupeleka Jeshi katika maeneo hayo ya masharika ili kulinda amani ya nchi hiyo vikosi vya kulinda amani vya Umoja wa Mataifa viliwasili mara maoja na vilibatizwa jina MONUSCO malengo muhimu muhimu ya MONUSCO yaliwekwa wazi mwanzoni tu wakati misheni hii inaanziswa ikiwa ni Ulinzi wa Raia, Msaada kwa Michakato ya Kisiasa, Upokonyaji Silaha na Uondoaji wa Silaha kwa vikundi vya uhalifu, Usaidizi wa Kibinadamu na Kujenga Uwezo kwa Majeshi ya DRC kwa bahati mbaya hadi leo malengo hayo hayaja fikiwa hata nusu na kinachoendelea ni historia ya vikundi vya uhalifu kuendelea kukita mizizi Raisi Joseph Kabila alihitimisha utawala wake kwa njia ya uchaguzi ambao ulikua ni wa mara ya kwanza kufanyika na kwa njia ya amani hii ilikua ni karibu miaka 60 tangia Taifa hilo lipate uhuru wake , wengi walipinga matokeo ya uchaguzi.Kumekuwa na tuhuma kali kwamba Raisi Mh Tshisekedi huyo mpya kuwa alifanya makubaliano ya nyuma ya pazia na Joseph Kabila, ambaye bado ana ushawishi mkubwa nchini humo. Hivi sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo inaongozwa na Raisi Mhe. Felix Tshisekedi mwanzo wa utawale wake Desemba 2018 alioneka ataweza kulifikisha Taifa lake pwana ya Amani inayosubiriwa kwa miongo kadha kinyume chake hali imezidi kuwa mbaya zaidi na makundi mbalimbali ya kiuhalifu yakipata nguvu katika upande huu wa mashariki mwa DRC kunakojumuisha majimbo ya Ituri, Kivu kusini na Kivu Kaskazini, kumesheheni makundi yaa waasi wenye silaha zaidi ya 100 na yanayojiendesha kwa kutumia rasilimali za taifa hilo.Kundi la waasi la M23, ndilo kuu lililobuniwa baada ya makubaliano ya kutafuta amani ya tarehe 23 Machi 2009. Kundi hili linaundwa na jamii ya Watusi walioko mashariki mwa Congo na Rwanda, pamoja na makabila kadha katika Kivu ya Kaskazini na Kusini, Kundi la M23, linatokana na Chama cha Kitaifa cha Ulinzi wa Watu - National Congress for the Defence of the People (CNDP).Kundi hili liliwahi kupigana na serikali kati ya mwaka 2006 na 2009. Serikali iliendesha harakati za kuwapokonya silaha, lakini baadaye harakati hizo zikasitishwa.Waasi wa M23 wanashukiwa kuwa wana uungwaji mkono na nchi ya jirani ya Rwanda wapiganaji hao walijipa jina la M23 baada ya mkataba wa amani wa tarehe 23 Machi 2009, uliotiwa saini na serikali na wanamgambo wa zamani wanaounga mkono Watutsi. kundi hilo limeanzisha mashambulizi mapya,na kukamata maeneo ya kimkakati Goma (Januari 2025), miji mikubwa zaidi mashariki mwa DRC kama Sake, Masisi, Babmbiro na Luberoo, maeneo hayo yalitekwa moja baada ya jingine kuanzia katikati mwa Desemba 2024.Wapiganaji waliteka miji hiyo muhimu, Sake ikiwa kilomita 23 kutoka Goma. Wiki chache zilizopita, M23 iliteka mji wa biashara wa Minova, na kupata njia muhimu za maeneo ya kiuchumi. M23 wamekiri kuendeleza mapigano yanayoendelea kipindi hiki wakikabiliana na wanajeshi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambapo zaidi ya watu 100,000 wametoroka makazi yao na maelfu ya watu kuuwawa. Ripoti nyingi za UN zinaonesha kuwa vitendo viovu juu ya raia wasio na hatia vimekua vikiongezeka kama vile ubakaji, mauaji ya halaiki na uporaji wa mali za raia hakika hakuna shaka kwamba operesheni za kijeshi zimeshindwa kabisa kuleta amani ya kudumu, na kwamba kuibuka tena kwa M23, kumewafanya watu wa mashariki ya Congo, kusalia katikati ya mzozo wa kivita. Umoja wa Afrika (AU)na ule wa kusini mwa jangwa la Sahara yaani (The Southern African Development Community –SADC) pamoja na Umoja wa Afirika wa masharika (The East African Community -EAC) tayari wamesha unesha juhudi zao za kutosha katika kutaka kutatua mgogoro huu hivyo nionavyo mimi ni vigumu kujitia chongo wakati macho yetu yote ni mazima ni lazima Bara la Afrika lizike tofauti zao na kuhakikisha tunasimama kidete wote kwa pamoja katika kusimika dhana ya kweli ya uadilifu bila kujali nani anatutizama ikiwa tutaendela kuweka mikakati ya kijeshi bila kukaa mezani na wanaodai kudhulumiwa yaani vikundi vya waasi hususa M23 basi ukoloni mambolea utaendelea kuitesa na kuiteka tena bara hili la Afrika. Nikiwa kama Muislamu tena niliyempokea Imamu wa zama Hadharat Mirza Ghulamu Ahmadi a.s ninawajibu zaidi ya kuwakumbusha viongozi wa Bara hili tukufu la kwa khera na mapenzi napende kuweka mbele ushauri na maoni ya kiongozi wangu mpendwa wa Jumuiya ya Ahmadiyya dunia Hadhart Mirza Masroor Ahmd atba katika sherehe za kuadhimisha miaka hamsini ya uhuru wa Tanzania bara katika salamu hizo aliweka bayana namna nzuri ya kulinda rasilimali na kuongoza Taifa lolote hususa nchi zinazo endelea alisema *"Ni maombi yangu kwamba watu hususan wa Tanzania na Afrika kwa ujumla waweze kutumia vilivyo faida ya uhuru walioupata. Wajitahidi kabisa kutumia raslimali walizopewa kwa ajili ya manufaa ya watu wao. Nchi zote ziweke maanani hadithi ya Mtukufu*

Endelea Uk wa 8..

MAJIBU YA BAADHI ZA SHUTUMA/PINGAMIZI DHIDI YA SEYYIDNA AHMAD[AS] KUWA KWAKE IBN MARYAM

بسم الله الرحمٰن الرحيم

Vivyo hivyo, Masihi Aliyeahidiwa[as] amelielezea kwa kina suala la kifo cha Nabii Issa[as] kwa njia mbalimbali ili watu waweze kuelewa. Moja ya njia zilizotumiwa na Masihi Aliyeahidiwa[as] ni kanuni ya lugha iliyotajwa hapo juu kwamba neno linalotumika kwa mtu anayerejea ni tofauti na lile linalotumika kwa mtu anayekuja au kwenda.

"Neno linalotumika kwa ujio wa Masihi ni 'Nuzool' na siyo 'Ruju'u. Kwanza kabisa, neno linalotumika kwa mtu anayerejea ni 'Ruju'u na neno hili halijawahi kutumika kwa Hazrat Isa (as). Pili, 'Nuzool' haimaanishi kuja kutoka mbinguni. Msafiri anaitwa 'Nazeel'. (Malfuzat – Juzuu-1, Uk-5 Imechapishwa tarehe 20 Agosti 1960).

Mahali pengine Masihi Aliyeahidiwa (as) anaandika:

أتظنون أنَّ المسيح ابن مريم سيرجع الى الأرض مِن السّماء؟ ولا تجدون لفظ الرجوع فِى كَلِمِ سيّد الرسل و أفضل الأنبياء۔ أَ أُلْهِمْتم بهذا أو تنحِتون لفظ الرجوع مِن عند أنفسِكم كَالخَائينين؟ وَمِنَ الْمَعلُوم أن هٰذا هُو اللفظ الخَاص الذى يُستعمل لرَجُل يأتى بَعْد الذَّهاب۔ و يتوجّه السَّفر الى الاياب، فهذا أبعدُ مِن أبلَغِ الْخَلقِ و امام الأنبياء أن يترک هٰهنا لفظ الرجوع و يَسْتَعْمل لفظ النزول ولا يتكلم كالفصحاء والبلغاء"(مكتوب احمد، روحانى خزائن جلد۔11، ص۔150, 151)

Tafsir: "Je, mnafikiri kwamba Masihi (as) mwana wa Maryam atarudi kutoka mbinguni kuja duniani? Ilhali neno 'kurudi' halipatikani katika kauli ya Bwana wa Mitume wote na Mbora wa Manabii wote s.a.w . Je, mmepokea ufunuo kuhusu hilo au mmebuni wenyewe kama wasio waaminifu? Inapaswa kujulikana kwamba neno hili hutumika mahsusi kwa yule mtu anayerejea kutoka kwenye safari. Kwa hivyo, haiwezekani kabisa kwa Mfasaha zaidi wa wote na Kiongozi wa Manabii wote kuacha neno 'Ruju`u' na kutumia neno 'Nuzool' na kutozungumza kama watu wa fasihi na walioelimika. (R.K. Juzuu-11 Uk: 150, 151)

Pamoja na marejeleo mengi kutoka kwa Quran, Hadith, na maandiko ya wanazuoni maarufu wa zamani na wa kisasa, mtazamo huu wa kiisilamu unaonyesha kuwa Hazrat Isa (as) harudi tena duniani. Kama ingekuwa hivyo, neno 'Ruju`u' lingetumika kwake badala ya 'Nuzool

Na dini zilizopita kwa mfano katika dini ya Nabii Nuhu a.s hazipingani na dini zingine kuhusiana na fikra hizi, basi hakika sisi tunakuta katika dini za kiyahudi yale yanayoashiria kurudi kwa Eliya nayeye anajulikana na katika dini ya kiislam, hakika kushuka kwake kutoka mbinguni itakuwa ni alama juu ya kuinuliwa masihi aliyeahidiwa kwa sababu yake kwaajili ya wayahudi na kwa wale waliokuwa wakimsubiri Masihi hivyo ndivyo yanavyopatikana yale yanayoeleza juu ya ujaji wa masihi a.s aliye ahidiwa kufika karne na karne ambaye anasubiriwa kwa shauku sana na dini zote kushuka kwake hapa duniani mara ya pili.

Na pia katika Islam kuna riwaya zinazoeleza kuhusiana na kushuka kwa Masihi na Imamu Mahdi, na kwa upande wa washia wanadai kuwa hivi karibuni katika zama za mwisho atarudi imamu aliyejificha kwenye pango ili auwe kila adui yake, na kwa hakika wafuasi wa dini hizi zote ambao wanasoma tabiri nyingi juu ya ujaji wa masihi Isa ibn Maryam kwa mara ya pili, hakika wao wanaamini kushuka kwake kutakuwa kwa mwili wake wa asili na nafsi yake ileile na hili ndio jambo ambalo linapingana na dini nyingine na hasa katika dini ya kiisilam ambayo inahukumu juu ya kutorudi aliyekufa katika maisha haya ya duniani mara nyingine.

Na kwa hakika alikwisha kufa Masih Ibn Maryam. Maelezo juu ya madhumuni haya ya kurejea kwa Nabii na akawaeleza wanafunzi wake kwamba kurejea kwa Nabii miongoni mwa Manabii maana yake si kuja kwa Nabii kwa nafsi yake na mwili wake ule ule , na hiyo inamaanisha ni kurejea kwa kiroho kwa maana kuwa atadhihirika mfano wa nabii atakae kuwa mfano wa yule aliyepita .

Pia Qur-an Tukufu ilipo bainisha, na hadithi sahihi ya kuwa Isa bin Maryam ameshakufa na hakika yeye hata rudi tena katika dunia hii, na inathibitika kwamba Masihi aliyeahidiwa anayesubiriwa yeye ni mtu mwingine atakae kuwa miongoni mwa Umma wa mtume saw. na ama kuitwa kwake Mashi Ibn Maryam basi ni kwasababu kufananisha kutokea katika sifa makhsusi , na hili ni jambo linalo julikana na lililo enea katika balagha na watu wa lugha, mara nyingi anapotajwa kwa kufananishwa na anafichika anaye fananishwa kwaye na kubadilika kufananishwa kwake ili kudhihirika kikamilifu mfanano kati ya vitu viwili, na inatambulika jina la anaye fananishwa kwaye juu ya anaye fananishwa kama anavyosema''Allamatul-Abdulkahiri al-jar Janii

'' hakika kufanana kumegawanyika kwa aliye bayana na asiye bayana. Basi kwa aliye bayana ya kuwa useme : kana kwamba zaidi ni simba basi unataja kila mmoja kati ya anaye fananishwa na anaye fananishwa kwake kwa jina lake, na ambaye si bayana ya kwamba amuangushe anayefananishwa katika ukumbusho na upeleke jina lake juu ya anaye fananishwa: kama kauli yake : uliona simba, unataka mtu anaye fanana na simba, ispokuwa wewe ubadilishe jina lake kwa kufikisha ujumbe ya kwamba hakuna hukumu kati yake na simba kana kwamba yeye amekwisha kuwa katika hali ya usimba kama jambo likiwa ndio hivi na wewe unafananisha mtu kwa mtu basi hakika wewe utakapo fananisha kitendo kwa kitendo hii itakuwa hukumu yake, basi wewe unasema tena kana kwamba upambaji wake wa maneno, basi unabainisha kwa anaye fananishwa na anaye fananishwa naye, na unasema tena kuwa yeye tu anasema sahihi unamfanya yeye kana kwamba yeye yupo katika uhakika.

Imamu Razi anasema katika tafsiri yake kuwa kutamkwa kwa jina la kitu juu ya yale anayo sababisha katika wingi wa umakhsusi wake na sifa zake inajuzu sana.

Na hivyo ndivyo masihi mauud a.s anamfanano mwingi kwa Masihi Issa ibn Maryam. Ndugu zangu wapendwa wasomaji wa Makala hii kwa heshma kubwa ningependa kuweka mbele yenu baadhi ya mifanano ya masihi wa islael na masihi wa sasa

1. Masihi ibn Maryam alikuja katika karne ya 14 baada ya Musa a.s na hivyo ndivyo alikuja masihi aliyeahidiwa katika karne ya 14 baada ya Mtume saw

2. Masihi wa wana wa Israel alikuwa ni muhudumu na msadikishaji wa sharia ya Musa na hakuleta sharia mpya ambayo ilikuja kufuta sharia iliyokuja kabla yake au kupunguza chochote, na hivyo ndivyo seyydna ahmad as aliponyanyuliwa kuwa Masihi na Imam Mahdi as akawa msadikishaji wa Qur-an Tukufu na mtumishi wa sharia ya Mtume Muhammad saw na wala hakuleta sharia mpya yenye kupunguza wala kufuta yale yaliyo kuwa kabla yake.

3. Masihi wa wana wa Isrsel alidhihiri wakati wa kutokea kwa udhaifu na kutofautiana na kuhitiiafiana kati ya maulamaa wa kiyahudi na hivyo ndivyo alivyokuja Masihin wa Muhammad s.a.w wakati wa udhaifu wa umma na kuhitilafiana kwa waislam na maulamaa au wanazuoni wa kiislam

4. Kama masihi wa wana wa Israel alivyo kuja katika siku za serikali ya kirumi na hivi ndivyo alivyokuja masihi wa Muhammad saw katika siku za serikali ya kiingereza na Mtume saw mwenyewe alisema neno Rumi juu ya wakristo kama alivyosema kiyama kitasimama na warumi watakuwa wengi sana { Muslim bab takum saat wa ruum akthar-nnasi}

5. Masihi wa wana wa Israeli alitumwa katika hali ya kawaida wala hakupata ufalme kinyume na madai ya wayahudi, na hivi ndivyo alivyotumwa Masihi aliyeahidiwa katika hali ya kawaida wala hakupewa ufalme wa kidhahiri katika hii dunia na alipewa kinyume na matamanio yetu ya kidhahili miongoni mwa waislam.

6. Masihi wa wana wa Israel hakuwa miongoni mwa Israel kwa upande wa baba, kwa sababu yeye alizaliwa bila baba na lakini yeye alikuwa mwisrael kwa upande wa mama. Na hivyo ndivyo masihi wa Muhammad s.a.w. hakutokana na waquraishi upande wa baba, lakini kwa upande wa mama alikuwa ni mquraishi kwasababu baadhi ya mama zake walikuwa ni miongoni wa Banuu fatma r.a ni sawa na kusema kuwa alikuwa ni miongoni mwa nyumba ya Mtume s.aw.

Itaendelea toleo Lijalo

Bustani ya Washairi

HONGERA TENA HONGERA

Ujumbe kwa Kaka ***Nasri Khalid M.*** Katika maisha mapya ya Ndoa.

Kwa jinale rahmani, utunzi niuanzie,
roho yangu tuliani, furaha nifurahie,
kaka yangu wa imani, tega sikio sikie,
hongera tena hongera, umetimu nusu dini.

Mkeo ni vazi jema, kutoka kwake manani,
nawe uwe mume mwema, nyumba iwe na amani,
pia umtunze vyema, mpe raha duniani,
hongera tena hongera, umetimu nusu dini.

Ubachera bai bai, sasa ni mume ndoani,
mkeo umsabahi, kwa upendo na utani,
furaha na kufurahi, awajazie manani,
hongera tena hongera, umetimu nusu dini.

Mola akujaalie, kizazi kilicho chema,
ridhiki akujazie, azidishie neema,
na shari azizuie, za waja waso wema,
hongera tena hongera, umetimu nusu dini.

Kuhusu kumlilia, rahmani mwenyezi,
kutwa kumsujudia, awape yake mapenzi,
simama usiku pia, kumuomba mwenyezi,
hongera tena hongera, umetimu nusu dini.

Uige mfano bora, waliokupa wazazi,
na ukawe mume bora, na pia baba mlezi,
imamu aliyebora, nyumbani uwe mlinzi,
hongera tena hongera, umetimu nusu dini.

Kituo nimeshafika, kalamu naweka chini,
na ujumbe umefika, kwa hilo ninaamini,
mi nduguyo sikufika, lakini nakuthamini,
h0ngera kaka hongera, umetimu nusu dini.

Mtunzi;
Yasri Bishazo (YABI_MSHAIRI)
Katoma Kagege (Bukoba Kagera)

JOHO LA SUBIRA
Hata muwe marafiki, wa kufa na kuzikana
Ipo siku ya mikiki, ya wawili kuagana
Ndivyo kapanga Maliki, ya kuwa na kuachana
Hivyo siku ikifika, vaa joho la subira.

Mahmood Hamsini Mubiru (Wamamba)
Kiwalani – Dar es salaam.

GIZA NA MWANGA
Matendo ya hadharani, nayo nyuma ya pazia
Aloruhusu Manani, kwa sisi sote insia
Hubagui asilani, yote hayo ni sawia
Na kama hiyo Siratwa, umepata ufaulu.

Na uwapo faraghani, machozi unayatoa
Kadhalika hadharani, katu huachi njia
Hofu yako ya moyoni, unamuhofu jalia
Ukitaka ufaulu, basi huo ufaulu.

Sura mbili ni motoni, ameyasema Rasua
Na ngarawa baharini, mawimbi yanatokea
Usimame kwa Imani, mwisho wa dhiki halua
Dhiki pamwe na faraja, Mletaji ni Kahari.

Mahmood Hamsini Mubiru (Wamamba)
Kiwalani – Dar es salaam.

RAFIKI

Thalatha wananitosha, rafiki nawathamini
Awali nakujulisha, kanileta duniani
Kunipa haya maisha, ni Mola wangu Manani
Ndiye Rafiki wa kwanza, Rabi aso mshirika.

Katiga wangu wa pili, ubora uso kifani
Katukuzwa na Jalali, yamo kwenye Qur'ani
Khatama wa Marasuli, mithili katu sioni.
Muhammad Muungamu, ndiyo siraja Munira.

Wa tatu sawa na mwili, sehemu yangu yakini
Ndugu zangu kwelikweli, wale wealioamini
Baridi na jua kali, pendo hadi kaburini
Na Inshallah hiyo kesho, peponi tuwe pamoja.

Na Mahmood Hamsin Mubiru –Wamamba Kiwalani - Dar es salaam.

Maisha ni mzunguko, ulipo kweko tatoka,
Wengine walikokweko, wewe huko utafika,
Kila siku badiliko, mwisho mauti tafika,
Tumia nafasi uko, sijutie ikitoka.

Mtunzi
Masihi Omary stambuli(Kisagwa)

PIGO KAVU

Binadamu pendo mbili, Njia dunia na Akhera
Ndo maumbile asili, Ongozo la kula dira
Maumivuye makali, Pigole li kavu Sana

Pendo moja kwa Rabana, Muumba mkidhi haja
Mfalme ndiye bwana, Mleta kila faraja
Kuishi Bila ya yeye, Pigole li kavu sana

Pendo upili dunia, Dhaifu la roho zetu
Twapenda vya kupotea, Jua hakidumu kitu,
Mwiba kwa mpenzi wako, Pigole li kavu sana

SHUNDA MSHUNDIA WANA
DALUNI, TANGA
Phone: +255656557721
Email: shunda267@gmail.com

SIKU YANGU.

Siku yangu kuzaliwa, Mimi kuja Duniani,
Wazazi walijaliwa, Furaha iso kifani,
Maombi nikaombewa, Ili nishi kwa Amani,
Mola ndo Akanikuza, Na wazazi kunilea.

Siku yangu ya sherehe, Kufurahi Duniani,
Yani raha Mustarehe, Kila kona Maishani,
Mola wangu nisamehe, Kutoka kwangu njiani,
Kweli nilifurahia, Mpaka kupitiliza.

Siku yangu kufariki, Kuondoka Duniani,
Itaacha taharuki, Wengi hawataamini,
Wapo wataohamaki, Vilio viso kifani,
Umati utafurika, Wa watu kujanizika.

Mtunzi:- Abubakary Abdallah Mwita.
Mkurya halisi.

TUPA

Ewe wadudi Mwenyezi, kwako ninakimbilia
Usopata usingizi, muumbaji wa dunia
Ni haya yangu majonzi, Rabi ninakulilia
Tupa ametangulia, Mola na umuhifadhi

Bakari Tupa kipenzi, asikari wa masia
Hakupata usingizi, kuhubiri jumuia
Pamwe na mzee N'ganzi, Na Ruwa hakusalia
Tupa ametangulia, Jalilu mpandishe ngazi

Jalilu mpandishe ngazi, Peponi patetulia
Kwani amefanya kazi, Mtiti pia wanajua
Na shekhe Shunda kipenzi, yeye pia analia
Tupa ametangulia, asikari wa masia

Enyi watanga wapenzi, muumpendao Jalia
Tupa ili tumuenzi, tuhubiri jumuia
Tuvirisishe vizazi, kuipenda ahmadia
Tupa ametangulia, Mola na umuhifadhi

Mie alwatani mlezi, Dua ninakuombea
Mola mughufiri mpenzi, peponi patetulia
Sifanyi tena ajizi, kuhubiri jumuia
Tupa ametangulia, Mola na umuhifadhi

AL-WATTANI _MLEZI
Rajabu Abasi Mkieti
Lusanga Muheza Tanga 15/8/2021

MUNGU WETU HANA DINI

Ndugu zangu habirini, wenye dini wapagani
Sikio niazimeni, mungu wetu hana dini
Chuki sababu ya dini, hutookoka motoni
Mapenzi yawe kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

Mmoja ulimwenguni, ndiye muumba wa wote
Mungu wa duniani, sayari na nyota zote
Mungu wetu hana dini, habagui vyake vote
Vilivyoko aridhini, hata vya mbinguni vyake.

Vyakuvila aridhini, wanyama nayo mimea
Hewa maji duniani, kila kitu cha tumia
Mungu wetu hana dini, tuache kujibagua
Kila kitu limwenguni, mahitaji akatoa.

Ubora ulimwenguni, binadamu akapewa
Atawale vya mbinguni, na akili akapewa
Mungu wetu hana dini, tutumie tulopewa
Sigombane kisa dini, utu ukapuuziwa.

Akaiweka na dini, Ili tuweze mtambua
Dunia iwe amani, kila kiumbe tulia
Mungu wetu hana dini, kazi kwetu kumjua
Dini hasa ni amani, salama kuwa dunia.

Utulivu duniani, upendo na usalama
Ndilo hasa dhumuni, yakujitendea wema
Mungu wetu hana dini, humpenda alomwema
Una dini mpagani, wengine wawe salama.

Acha nifike mwishoni, akili mekufunguw,
Mungu wetu hana dini, acheni kujibaguwa
Kama kafiri kwa dini, kimaisha takutowa,
Tupendane bila dini, kituacha metugawa

Masihi Omary Stambuli

Mazungumzo ya Hekima kati ya Mtu na Punda

Kulikuwa na siku ya kawaida nilipoamua kwenda mbali na kelele za mjini, kutafuta muda wa kupumzika katika sehemu ambapo nisipate watu ambao huwa wanajifanya kuwa wanye elimu nyingi. Niende mbali na hekaheka za watu na fujo zao.

Nikafika shambani ambapo karibu na mti punda mmoja alifungwa na kamba. Nikamsogelea na nikakaa karibu naye na nikasema:



Mtu: Wewe punda, binadamu huwa wanakucheka na kukusema kwamba wewe ni mpumbavu je, huu ni ukweli?

Punda: (Kwa kutabasamu) kwa kweli mimi sijawahi kudai kwamba nina akili hata hivyo sijawahi kusema uongo wala kufanya hiana wala kumdhuru yeyote. Je, huu ni upumbavu? Je, unapenda na mimi pia niendelee kuwa ndumi la kuwili?

Mtu: B i n a d a m u wanakuona wewe huna faida bali wewe ni kifaa cha kubeba mzigo tu.

Punda: Mimi huwa sizungumzi sana lakini ninabeba mizigo mizito lakini wapo binadamu ambao wanaongea sana bila kubeba mizigo.

Mtu: Je, huchoki na hiyo kuwa unafanya kazi kubwa na unakaa kimya?

Punda: (Akaitikia kwa kichwa) bila shaka uchovu ni sehemu ya maisha lakini sijali sana wala sivunjiki moyo. Changamotohuwa hazimshindi yule anayekubaliana nazo kwa bashasha. Lakini zinamshinda yule anayeendelea kupambana nazo kwa uongo. Mimi nina kazi ya kubeba mzigo na kukaa kimya; lakini kwa bahati sijapewa kazi ya kudanganya, kufanya hiana au kusema uongo. Wapo binadamu ambao wanatingwa na mtihani wanapotumia udanganyifu, hiana na uongo katika maisha yao.

Mtu: N i n i mtazamo wako kuhusu maisha?

Punda: K w a kweli maisha si rahisi, yana milima na mabonde, lakini hata siku moja hayaturuhusu kuwadhuru wengine au kuwadanganya au kuwachukia.

Mtu: Hapo nikaanza kufikiria kwamba kwa kweli mazungumzo yake yana hekima kubwa sana na nikawaza sura za binadamu katika nafasi mbalimbali ambao wana upungufu huu. Mawazo yangu yakamfikia kiongozi wa dini anayesisitiza sana kutumia unyenyekevu lakini akielekezwa na watu wengine anawasha moto wa hasira. Kisha nikamwaza mwanasiasa fulani ambaye hutoa hotuba nzuri juu ya haki za binadamu lakini yeye mwenyewe hatimizi wajibu wake. Pia, nikafikiria kuhusu vijana ambao humcheka punda lakini wenyewe hawamjui punda anavyoweza kuwa na maneno ya hekima.

Mtu: Ukisema upendo unamaanisha nini?

Punda: (Kwa kutabasamu) upendo ni jambo zuri sana. Mimi ninapenda ardhi ninayoikanyaga, ninawapenda watu ambao wananichunga machungani na saa nyingine wananipiga kwa nguvu hata hivyo nawapenda, ninawapenda watu wanaoninywesha maji bila kuniuliza kabila langu. Kwa hiyo upendo na mapenzi haviishii kwenye mashairi na nyimbo za binadamu tu bali upendo halisi ni kuwa mwaminifu hata kama hauthaminiwi sana, upendo halisi ni kuongea kwa upole hata kama watu wakucheke au wakutendee vibaya.


Mtu: Je unatamani kuwa binadamu?

Punda: Mimi nikipewa nafasi nitabaki kuwa punda tu. Siwapendi binadamu ambao wanaona mambo kijuujuu tu na hawazami chini kupata hekima yake. Mimi sipendi mizozo ya binadamu inayoanza kwa mdomo na inapelekea kumwaga damu. Mimi ni punda ambaye sina misimamo miwili wala sina rangi mbili.

Mtu: Aisee, ni kweli una mawazo mazuri. Ina maana hulalamiki kuwa uliumbwa kuwa punda?

Punda: H a p a n a , ikumbukwe usiniulize kwa nini mimi niliumbwa kuwa punda bali ujiulize kwa nini wewe haujabaki kuwa binadamu.

Ijapokuwa hadithi hii ni ya kubuni tu lakini inaeleza jambo kubwa sana kuwa sisi binadamu tusisahau kutendeana kwa ubinadamu. Tunatakiwa kuishi kwa kupendana sana. Vinginevyo tutaporomoka katika maadili na kukosa sifa.



UBUYU WA ROJO

MAHITAJI:

-UBUYU WA MBEGU
-UNGA WA UBUYU
-SUKARI
-IRIKI YA UNGA
-PILPILIMANGA YA UNGA



Andaa maji kwenye sufuria, kisha weka mahitaji yako yote kwenye sufuria.
Kisha bandika jikoni, acha uchemke mpaka kubaki hilo rojo kama hapo unaweza kupaka kwenye vikopo au vifuko vya **ice cream.**

NAUWEKA KWENYE FRIJI UPATE BARIDI
Hazina ulazima wa kuganda watoto wanapenda ivo ivo tu.

BIASHARA NZURI KAMA NI MAMA UPO NYUMBANI
HUKOSI HELA

JUHUDI NA VIKWAZO KATIKA KUIPATA AMANI YA CONGO DRC.

Kutoka 04

Mtume Muhammad s.a.w. isemayo: Kiongozi wa nchi ni mtumishi wa Taifa. Hili ni jambo muhimu la kukumbukwa, sheria zote zinazotengenezwa katika nchi ziwe sawa kwa watu maskini na matajiri, jambo hili likifuatwa basi, Inshallah - Mwenyezi Mungu Akipenda - uhuru ambao mmeupata baada ya muda mrefu sana wa ukoloni na utumwa sasa utadumu. Lakini endapo hamtalifuata hili mataifa makubwa kwa mara nyingine tena yataingia katika nchi zenu na kuchukuwa malighafi zenu kupitia mipango ya udanganyifu na hila ama kwa sababu zozote ziwazo zisizo na ukweli ndani yake. Kama viongozi wa nchi zinazoendelea wanatimiza haki za watu wao na watu wenyewe wanatoa kipaumbele kwa maslahi ya taifa lao hapana shaka taifa litaendelea. Inshallah – Mungu Akipenda.Hapana shaka kama nchi zote za Afrika zitachukua njia hii kwa hakika Afrika itapiga hatua kubwa ya maendeleo tena kwa kasi kubwa.Nina uhakika kabisa kwamba, kama nchi za Kiafrika na watu wake wataungana na kutimiza yale yote yanayotakiwa na adili basi siku moja bara la Afrika litaibuka kuwa taifa lenye nguvu duniani. Tunamuomba Mwenyezi Mungu hili liweze kutokea. Inshallah"

Ukhalifa- Chanzo cha Baraka Zote

Kutoka Uk> 11

kulala kila usiku na kuwaombea dua hata wakati ninapoamka.

Hazrat Hakim Maulana Nuruddin ra. Alitoa mwongozo akisema: "Mtu anaweza kujifunza mambo mengi kutoka kwa nyuki, anasema nyuki hakai juu ya uchafu kisha anakuwa mtiifu kwa malkia wake. Ina maana kila mmoja wetu ajisafishe na kujitakasa na uchafu wa namna yoyote, madhambi na maovu ya aina yote pia ni uchafu kisha ninasema ukitoka nje ya utii wa Khalifa pia ni sawa sawa na kukaa juu ya uchafu."

Hazrat Mirza Bashir Ahmad mdogo wake Hazrat khalifa wa pili ra anasema siku moja akaja mtu mmoja na kuanza kunielezea upungufu wa afisa moja wa Jamaat nami niliendelea kuyasikiliza maneno yake hadi aliposema nitamshitaki kwa Khalifa ndipo nikashutuka na kumzuia. Kisha nikamwambia kuwa bwana unaweza kumwandikia Khalifa na ni muhimu kumjulisha Khalifa habari za Jamaati lakini usimpelekee Khalifa malalamiko kumhusu mtu yeyote; ukiamua kufanya hivyo basi ninakuomba kutafakari zaidi ya mara elfu moja kabla ya kumwandikia Khalifa. Ndugu zangu, hizi ni miongoni mwa adabu za kupeleka taarifa yoyote kwa Khalifa nasi tunatakiwa kuzishika kila siku.

Hazrat Musleh Maud ra. Alisema: "kumbukeni ya kuwa maendeleo yenu yote yanapatikana katika kujiunga na ukhalifa na siku ambapo mkisahau jambo hili na kughafilika nalo basi siku hiyo itakuwa siku yenu ya mwisho. Lakini endapo mtaendelea kushikamana na Ukhalifa basi lau kama watu wa dunia nzima wakiamua kuwaangamizeni hawataweza kufanya chochote.

Seyyedna Ahmad a.s. anasema: "Malaika na roho takatifu hushuka katika wakati ambapo mtu adhimu anaposhuka ardhini akivaa taji la ukhalifa na kupata maneno ya Mwenyezi Mungu. Yule khalifa hupewa roho takatifu hasa na wale malaika walio pamoja naye hushushwa kwa watu wenye bahati.
(Fat-he Islam, uk. 12. *Maelezo ya chini*)

Lazima tuwe na uhusiano wa karibu na wa uaiminifu mkubwa na Khalifa ili tupate faida ya malaika. Hazrat Musleh Maud r.a.alisema akieleza jambo hili kuwa:

"Njia mojawapo ya kujipatia baraka za malaika ni kujenga uhusiano na uaminifu kwa makhalifa waliochaguliwa na Mwenyezi Mungu na kuwatii ……. kuwa na uhusiano na makhalifa wa kweli kunazalisha udugu na malaika na kumjaalia mtu apate nuru za Kiungu."
(Tafsire Kabir,J.2.uk.561)

Khalifa wa nne alieleza hekima hii kuwa;

Ningependa kueleza kwamba nimeshashuhudia na hata mbele pia itatokea hivi kuwa, kama mwahmadiyya yeyote haheshimu cheo cha ukhalifa, hampendi kikweli, na hana udugu wa moyo naye basi maombi yake hayatapokelewa yaani maombi ya khalifa hatapokelewa kwa ajili ya yule mtu. Maombi ya Khalifa yatapokelewa kwa ajili ya yule tu anayemwandikia barua kwa uaminifu." (Al-Fazl, 27 Julai 1982)
Mwenyezi Mungu Atuwezeshe sisi sote kumtii kikamilifu Khalifa wa zama na kujenga naye uhusiano wa dhati kabisa. Aamiin.

MATUKIO KATIKA PICHA

AHMADIYYA MUSLIM COMMUNITY

STATEMENT OF CONDOLENCE ON THE DEATH OF POPE FRANCIS

I was deeply saddened to learn of the passing of His Holiness Pope Francis. Throughout his life, Pope Francis sought to serve the poor and vulnerable, demonstrating immense sympathy for those suffering under the heavy weight of warfare, persecution, and injustice. He was a man of compassion, humility, and faith who strived to build bridges between people of different faiths and beliefs.

During his Papacy, Pope Francis received representatives of the Ahmadiyya Muslim Community with warmth and grace at the Vatican, for which we will always be grateful.

On behalf of the Ahmadiyya Muslim Community, I extend our sincere condolences to the Catholic Church and its members around the world.

Yours sincerely,

MIRZA MASROOR AHMAD

Khalifatul Masih V
HEAD OF THE WORLDWIDE
AHMADIYYA MUSLIM COMMUNITY

WWW.PRESSAHMADIYYA.COM



Maswali kutoka katika kitabu cha

Makusudio 23 Adhimu ya ujenzi wa Baitullah

Uk. 26,27. 36. Kusudio la kumi na moja la ujenzi wa Baitullah ni nini?

Jibu:ilivyoandikwa katika neno Tahhiraa Baitiyya طهرا بيتى yaani kupitia nyumba hii watu watajifunza kuweka usafi wa dhahiri na wa kiroho

Uk. 27. 37. Kusudio la 12 la ujenzi wa Baitullah ni nini? Jibu:lililoandikwa katika neno lttwaaifiina لطائفين yaani wawakilishi wa mataifa yote ya ulimwengu watajumuika hapa mara kwa mara.

38. Kusudio la kumi na tatu la ujenzi wa Baitullah ni nini? Jibu: lililoandikwa katika neno wal'akifiina والعاكفين maana yake kupitia hii izalike kaumu watakaojitolea wakfu maisha yao katika njia ya Mwenyezi Mungu na kutimiza makusudio ya Baitullah.

39. Kusudio la 14 la ujenzi wa Baitullah ni nini?

Jibu: lililoandikwa katika neno {wa rukka 's-sujuud} وركع السجود ili iumbwe kaumu wawe imara sana kwa imani ya Umoja wa Mungu na waishi maisha yao yote kumtii Mungu na kujitupa kwake.

Uk.27,28 40 Kusudio la 15 la ujenzi wa Baitullah ni nini? Jibu: Kusudio la kumi na tano ndilo بلدا آمنا Baladan Aaminan (Mji wa amani kwa kila namna) Katika maneno hayo Mungu alituambia kwamba tutaihifadhi nyumba hii na mashambulizi ya kidhuluma ya dunia na washambulizi wataangamizwa,na Nabii na sheria yake na pia italindwa kwa kila namna na itadumu milele.

Uk.28 41.Kusudio la 16 la ujenzi wa Baitullah ni nini?

Jibu: Kusudio la kumi na sita ni Warzuk ahlahu minaththamarati وارزق اهله من الثمرات Yaani watu watakaojitolea kwa ajili ya Baitullah watapata baraka kubwa na natija bora.

42. Kusudio la 17 la ujenzi wa Baitullah ni nini? Jibu. Kama alivyosema Allah kwamba Rabbana takabbal minna Ili watu wajue kivitendo njia ya kujipatia daraja za juu za ruhania ni dua pekee. katika kuomba dua mtu anapofikia upeo wa kujinyenyekeza na kutiririsha machozi na hali ya mauti inazalika ndipo fadhili ya Mungu huteremka na mja anafunguliwa njia za maarifa.

Uk.29 43.Fadhili na baraka ya Mwenyezi Mungu huvutwa na nini?
Jibu: Zinavutwa na kudumu na maombi kwa unyenyekevu.

44. Kusudio la 18 la ujenzi wa Baitullah ni nini? Jibu: Kusudio la 18 ni katika neno Samii . Hii ni sifa ya Mwenyezi Mungu maana yake anayesikia na kuitikia. Hapo Mungu anasema kuwa watakaoomba wataona kwamba ninawasikia na kubali maombi yao sana.

Uk.30. 45. Kusudio la 19 la ujenzi wa Baitullah ni nini? Jibu: kusudio la 19. Ili watu wapate ujuzi wa sifa ya Mungu ijulikanayo 'Aleem علیم. Yaani Mjuzi sana. Kwa kuwa wanadamu hatuna ujuzi sana na mambo na anayejua kila kitu ni Mungu pekee kwa hiyo baadhi ya wakati tukiomba jambo fulani litakaloleta madhara fulani Mungu kwa elimu yake hatokubali vile tutavyotaka bali maombi hayo atakubali kwa namna ambavyo itufaidi zaidi kwa sababu yeye ndiye Aleem yaani mjuzi sana.

Uk.30,31 46. Kusudio la 20 la ujenzi wa Baitullah ni nini? Jibu: Kusudio la 20 ni لک ومن ذريتنا امة مسلمة wamin dhurriyyatinaa ummatan muslimatan laka Yaani ili watu waige na wafuate mwenendo na khulka za Nabii Ibrahim AS na mwanaye yaani baba na watoto wake pia wajitolee na wajitupe mbele ya Mola wao. Yaani kaumu hii wataendelea kusihi na kuwalea vizazi vyao ktk njia ya Allah mtukufu.

47. Kusudio la 21 la ujenzi wa Baitullah ni nini?
Jibu: Kusudio la 21 ni ارنا مناسكنا Arinaa manaasikanaa maana yake ni Atakapokuja Mtume SAW ataleta sheria kamilifu timilifu itakayotimiza mahitaji yote ya kumwabudu Mwenyezi Mungu.

Uk.32 48. Kusudio la 22 la ujenzi wa Baitullah ni nini? Jibu: Kusudio la 22 iko kwenye neno Tub 'alaina تب علينا utusamehe madhambi yetu maana yake kupitia nyumba hii wapatikane watu watakaojua kwamba pasipo tauba na kuomba msamaha na madhambi hawawezi kupata maarifa ,kwa hiyo waaminio watadumu kutubu na kuomba ghofira.

Uk.32,33 49. Kusudio la 23 la ujenzi wa Baitullah ni nini? Jibu: Kusudio la 23 iko katika Maneno yafuatayo:ربنا وابعث فيهم رسولا منهم Rabbanaa wab 'ath fiihim rasulan minhum ili sehemu hii iwe mahali ambapo mja maalum wa Allah mtukufu atakuja atakayepata daraja ya kusifiwa sana, atakayekuwa Mbora wa Mitume

Uk. 40 50. Wakati gani mataifa yote yalianza kujua Baraka na neema za Baitullah ?

Jibu:Alipodhihiri Mtume Muhammad Swallalaho alaih wasallam.

Uk. 41 51. Jambo gani ilikuwa muhimu litokee ili ahadi ya Mungu aliyofungana na Nabii Ibrahim itimie? Jibu: ilikuwa muhimu kuteremka Sheria ya mwisho iliyokamilika ndio maana Quran tukufu inasema mwanzoni Dhalikal kitabu. Hicho ndicho kile kitabu mlichokuwa mnakisubiria.

Uk.42 52. Kuna tofauti gani kati ya vitabu vilivyoteremka kabla na Quran tukufu?

Jibu: Hadhrat Masih Aliyeahidiwa AS alisema kwamba Vitabu vingine havina dalili na maarifa kama sura moja yaani Surat Alfatiha sembuse vikabiliane na Quran yote.

Uk.43 53.Sifa ya Quran tukufu ni La Raiba Fiihi yaani haina shaka yoyote ina maana gani ?

Jibu: Yaani inaondoa kila dhana na wasiwasi (Shaka) kwa sababu Quran inapoleta jambo lolote inatoa dalili na ishara bayana na kila mwongozo na ukweli unaolazimika kuemo ndani ya kitabu kikamilifu haukosekani ndani yake.

Uk.44 54.Toa dalili moja kuwa Quran tukufu ni kitabu kikamilifu ?

Jibu: Kila ukweli na maarifa ambayo kitabu chochote kingine kinaweza kudai imo ndani ya Quran tukufu na pia zimo ndani yake kweli na maarifa mengine mengi yasiyomo ndani ya Vitabu vingine.

Uk.45 55.Tunawezaje kuwa Ummati Bora ?

Jibu:Tukitekeleza mafundisho ya Mtume Muhammad SAW na Maisha yetu yaendane sawa na sheria yake ndipo kuwanufaisha wanadamu wote na kuwa Umma Bora.

Uk.46 56.Toa Tafsiri ya كنتم خيرامة اخرجت للناس kuntum Khairu ummatin Ukhrijat linnas ?

Jibu: Ninyi ni umma bora mlioumbwa kwa manufaa ya wanadamu.

Uk.47 57.Quran tukufu ina maagizo na makatazo yasiopungua 700 na vitabu vingine vina hukumu chache sababu yake ni nini? Jibu: kwa sababu vipawa na vipaji vya watu wa zamani visingeweza kubeba hukumu zote kama wafuasi wa Mtume Muhammad SAW

Uk.49 58.kamilisha sentensi : Islam imefutilia mbali kila ubaguzi na tofauti baina ya … ? Jibu: Islam imefutilia mbali kila ubaguzi na tofauti baina ya mtu na mtu na hivyo ikaimarisha heshima na adhama ya binadamu.

Uk.51 59.Toa Tafsiri ya la tuzakku anfusakum huwa a'alamu bimanittaqa…(SURA AN_NAJM AYA 33) لاتزكوا انفسكم هواعلم بمن اتقى ? Jibu: Basi msijitakase nafsi zenu, yeye anamjua sana aliyetakasika.

Uk.52 60.Kamlisha sentensi: katika kila kaumu wapo wenye ustadi mzuri na vipaji
Jibu: katika kila kaumu wapo wenye ustadi mzuri na ndani ya kila kaumu kuna vichwamaji pia.

Uk.53 61.Kamilisha sentensi: Islam haipendi ubaghuzi…Jibu: Islam haipendi ubaghuzi ,bali inaimarisha usawa.

Uk.54 62.Dini ya Islam imetufundisha nguzo tatu kwa usawa wa binadamu ,uzitaje?
Jibu : 1.Uadilifu 2.Hisani 3.Iitai dhilkurbaa (kama afanyavyo mama au ndugu wa karibu)

Uk.61 63.Tangu lini Baitullah ilianza kupendwa na kufanyiwa ziyara kutoka mataifa yote?

Jibu: Baada ya kufika Mtume Muhammad SAW na sheria yake tukufu.

Uk.61,62 64.Neno Mubarak lilipokuja kwa ajili ya Baitullah lina maana mbili ,ufafanue? Jibu:1. Baitullah itakuwa ni makazi wawakilishi wa mataifa yote ya ulimwengu na watu kutoka mataifa yote wanaendelea kujumuika hapo. 2. Baitullah na mji wake utakuwa mahali pa kuzalika sheria moja ambamo zitajumuishwa kweli zote za kimsingi na miongozo yote vinayopatikana katika sheria zote za manabii wote.

Uk.63 65.Toa Tafsiri ya Sura an'aam aya 156 inayosema: wa Hadha kitabun anzalnaahu mubarakun fattabiuuhu wattaqu la'allakum turhamuun. وهذا كتاب انزلناه مبارک فاتبعوه واتقوا لعلكم ترحمون
Jibu: Na hiki ni kitabu tulichokiterem sha,kilichobarikiwa,basi kifuateni na ogopeni ili mrehemiwe.

66. Quran tukufu inaeleza faida gani kufuata Sheria hii ya mwisho.? Jibu:1. mkifuata sheria hii mtaingia katika hifadhi ya Mungu naye atawakingeni na wasiwasi wote wa kishetani.
2. Faida ya pili mtastahili kurehemiwa na Mwenyezi Mungu na mtapata ustawi wa kimwili na kiroho.

Uk.64 67.Kwa ajili ya Baitullah na sheria iliyoteremka yalikuja maneno Hudan lil aalamiin,maana yake nini? Jibu:Itakuwa mwongozo kwa walimwengu wote.

Uk.65 68.Toa tafsiri ya Sura Almaida aya 4 اليوم اكملت لكم دينكم واتممت عليكم نعمتى ورضيت لكم الاسلام دينا
Al yauma akmaltu lakum dinakum wa atmamtu alaikum ni'mati wa radhitu lakumul islama diina. Jibu:Leo tumewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema yang una nimewapendeleeni Islam iwe dini yenu.

Uk.66 67.Je , kuna madai ya ukamilifu wa sheria katika Agano la kale au agano jipya ?
Jibu:Hapana ,Hakuna Kitabu kabla ya Quran kilichodai madai hayo. Kwa mfano
Yohana 16 _ 12 hadi 20 inayosema: Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena.

68.Maneno yaliyoambiwa katika Yohana 16 _ 12 hadi 20 maana yake ni nini? Jibu: Maneno haya yanaonyesha kwamba wakati wa yesu watu hawakuwa na uwezo kuelewa mambo yote na injili inabashiria hapo ujaji wa Sheria kamilifu baada yake.

Uk.67 69. Katika Sura Bani Isra iil aya 82 ilikuja jaa- al hak wa zahakal batil Katika aya hii , neno hak ina maana gani.? Jibu: 1. Dhati ya Mwenyezi Mungu 2. Mtume Muhammad SAW 3. Qur'an Tukufu

Uk.69 70. Ni nini mwongozo kwa walimwengu wote? Jibu: Qur'an tukufu
70.Kamilisha sentensi Akili yenyewe ni kipofu tu Kama… Jibu: Akili yenyewe ni kipofu tu kama hakuna jua la ufunuo.

Uk.71 71.QAYYUM ni sifa ya Mungu maana yake ni nini? Jibu:Mhifadhi wa Milele

Uk.73 72. Mtu akipata daraja kubwa la Takwa akawa mcha Mungu kwelikweli, Quran Tukufu inamsaidia nini? Jibu: Quran Tukufu inamfungulia njia nyingi zaidi za takwa sawa na ahadi yake kuwa هدى للمتقين MWONGOZO KWA WAMCHAO.

Uk.74 73. Mtu anapata faida gani kumsalia Mtume Muhammad SAW? Jibu: Mtu anayempenda Mtume Muhammad SAW na kumsalia yaani kumtakia baraka ,rehema na usalama basi Mungu naye atampatia huyo mwombaji sehemu fulani za rehema baraka na usalama naye anapata mapenzi ya Allah.

Uk.75 74.Kuna faida gani kumwamini , kumpenda na kumfuata Mtume Muhammad SAW ?
Jibu: Anayempenda na kumfuata Mtume Muhammad SAW wanapata nuru ambayo inawaongoza na kumwangazia njia za ruhania na baraka na rehema ambazo hazina mipaka na hizo zote hazitengani naye hadi kiyama.

Ukhalifa- Chanzo cha Baraka Zote

Kutoka uk. 12

mbele gurudumu la maendeleo ya dini na kukamilisha kazi za nabii wake chini ya uongozi na msaada wa Mwenyezi Mungu. Katika makala hii nitatoa maelezo zaidi juu ya kudra ya pili ya Mwenyezi Mungu, inayoitwa Ukhalifa wa nabii.

Bwana wetu mtume mtukufu Muhammad[saw].alisema:

مَا كَانَتِ النُّبُوَّةُ قَطُّ اِلَّاتَبِعَتْهَاخِلَافَةٌ.

Tafsiri: hakuna unabii katu ila ukhalifa unaufuata.

(Kanzul Ummal,Al-Faslul Awwal, hadith no.3224)

Ukhalifa ulipatikana baada ya kila unabii na kama mfumo huu wa ukhalifa usingepatikana katika wafuasi wake basi kazi ya nabii ingeweza kuharibika. Shabaha na lengo la kuja kwa nabii lisingeweza kutimia barabara na watu ambao walipata malezi na nabii huyu wangeweza kupotea. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu Alianzisha ukhalifa kila baada ya kufariki kwa nabii ili baraka zake za kiroho zidumu milele. Hivyo neema ya ukhalifa ni kubwa zaidi baada ya neema ya unabii kwa ajili ya waaminio.

Ukhalifa katika Qurani Tukufu

Ukhalifa wenye baraka tele na heri nyingi umebashiriwa na kuahidiwa ndani ya Kurani Tukufu. Umuhimu wa nidhamu ya ukhalifa pamoja na baraka zake na wajibu wetu kutokana na ukhalifa umebainishwa na Mwenyezi Mungu katika aya 56 na 57 za sura al Nuur sura namba 24 kwamba:

''Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na chochote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri. Na simamisheni sala na toeni zaka na mtiini mtume ili mpate kurehemiwa".

Mwenyezi Mungu Amefafanua kinagaubaga ndani ya aya hizi kwamba makhalifa watapatikana kati ya waaminio kama walipatikana miongoni mwa wale waliokuwa kabla yao. Ndiyo maana tunasema kwamba ukhalifa unakuja kukamilisha nuru ya Mtume na kuidumisha milele pamoja na kupeleka mbele mwongozo na rehema inayoshuka kwa Mtume. Mtu huyu yaani anayeshika nafasi ya mtume anaongeza neema za kiungu na mafundisho ya nabii na imani na vitendo vizuri vya waaminio kwa msingi uliowekwa na Nabii kwa msaada maalum wa Allah Subhanahu wa Taalah.

Ndani ya aya hizi Mwenyezi Mungu Amewaahidi waaminio kwamba ukhalifa utapatikana kati ya wale tu ambao wanamwamini Mwenyezi Mungu na kufanya vitendo vizuri. Ukhalifa ulipatikana kati ya waislamu mara baada ya Mtume S.A.W kwa mujibu wa aya hii. Utaratibu wa ukhalifa ukaendelea kwa miaka 30 sawa na bishara ya Mtume Muhammad saw. Kisha Ukhalifa wa namna hii ulianzishwa tena ndani ya Jumuiyya ya Waislamu Waahmadiyya.

Umuhimu na adhama ya Ukhalifa

Hazrat Seyyid Ismail shahid r.a. aliandika:

"Uimamu uliokamilika unaitwa Khilafat-e-Rashida, Khilafat aala minhajun nubuwwat na Khilafat-e-rehma. Ibainike kuwa nuru ya uimamu ilipoingia kwenye kioo cha Ukhalifa basi neema ya kiungu ilikamilika kwa ajili kuwalea binadamu kwa ukamilifu wa kiroho pamoja na rehema kamili ya Mrehemevu uling'aa kuwa nuru juu ya nuru." (Mansab-e Imamat, kur. 82-83)

Imam-uz-Zaman Seyidna Ahmad[sa] anasema:

Maana ya khalifa ni naibu; ambaye hujadidisha dini. Wale watu wanaokuja kuliondoa giza linaloenea baada ya kuondoka kwa manabii, huitwa makhalifa. (Malfuzaat j.4 uk. 383).

Pia, anasema akieleza zaidi:

''Khalifa anakuwa naibu; na naibu wa Mtume kwa maana halisi ni yule tu ambaye anakuwa na sifa na tabia ya Mtume, kwa sababu Mtume saw hakuwaita wafalme wadhalimu kuwa makhalifa kwani khalifa anakuwa *dhill* yaani mfano halisi wa nabii, na kwa sababu mtu yeyote hawezi kuishi milele, kwa hiyo Mwenyezi Mungu alipenda kwamba manabii ambao ni bora kuliko watu wote wa dunia hii, waishi kwa njia ya mfano. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu Alipenda utaratibu wa ukhalifa uendelee ili watu wa dunia wasikose baraka za utume muda wowote.'

Hazrat Mirza Bashir Uddin Mahmud Ahmad (Khalifatul Masihi wa Pili r.a) anasema:

"Maana ya Khalifa ni kwamba neno lolote likitoka kutoka mdomo wa Khalifa basi palepale sisi tuache mipango yetu yote, mapendekezo yetu yote na rai zetu zote, kisha tuelewe kwamba sasa utafaa mpango ule tu, pendekezo lile tu na rai ile tu iliyotolewa na Khalifa, bila ya kujifunza hii, hotuba zote ni bure, mipango yote ni batili na kazi zote hazitafaa.

(Hotuba ya Ijumaa ya 24 Januari 1936).

Pia, aliwahi kueleza maana ya Jamaat (jumuiya) kwamba:

"Maana ya Jamaat ni hii kwamba watu wawe wanaongozwa na imamu mmoja. Wale watu hawako chini ya imamu (mmoja) sio na Fadhili za Allaha haziwashuki zinazowashukia wanajamaati." (Anwar ul Uloom, J.2. uk.13)

Cheo cha Khalifa

Hazrat Mirza Bashir Uddin Mahmud Ahmad r.a anasema:

"(mtu) ambaye Mungu Anamwambia matakwa yake, ambaye Mungu Anamshushia funuo zake, ambaye Mungu Amemteua kuwa imam na khalifa wa Jamaat, mnaweza kuzitekeleza shughuli zenu kwa kushauriana naye na kwa kupata mwongozo wake. Shughuli zenu zitabarikiwa jinsi mtakavyojiunganisha naye na shughuli zenu zitakosa baraka kadiri mtakavyokaa mbali naye. Kama tawi lile tu linaweza kuzaa matunda ambalo linaendelea kuunganana mti na tawi lililokatwa na kutupwa mbali na mti haliwezi kuzaa matunda, hali kadhalika mtu yule tu anaweza kufanya kazi ya Jumuiya hii anayejiunganisha na imamu. Kama mtu yeyote hajiunganishi na imamu hata kama anajua elimu zote za dunia, hawezi kufanya kazi ya Jumuiya hii zaidi kuliko mwanambuzi. (Al-Fazl, Qadian. 20 nov.1946).

Hazrat Seyyid Ismail Shahid r.a. alisemaa akieleza daraja la Imam:

"Imam ni kama mwana aliyebarikiwa wa Mtume, na wakuu wote wa umma na watawa (watukufu) wote wa dini ni kama wafanyakazi, wahudumu, watumishi na watumwa waaminifu (mbele yake)…kwa ufupi bila kumpitia yeye wazo la kupata ukaribu na Mungu ni wazo batili na ni mawazo ya bure yasiyokubaliwa na kukataliwa tu."(Mansabe Imamat,uk.78).

Wale watu wanaoanza kujifananisha na Khalifa wa Zama wanapaswa kuyatilia manani maneno yafuatayo ya Hazrat Seyyid Ismail Shahid r.a. kuwa:

"Kushindana naye ni sawasawa na kushindana na Kudra ya Mungu, na kumpinga yeye ni kama kumpinga Mungu Mwenye Uwezo, kila ubora na sifa isiyotumika kwa ajili ya kumhudumia yeye ni fikra mbovu na kila elimu isiyotumika kwa ajili ya kubainisha adhma na shani yake ni bure tu. Kila mwenye sifa anayetaka kujilinganisha naye anashika njia ya kumshirikisha Mungu, hii ndio alama mojawapo ya wenye sifa kwamba wadumu katika kumtumikia yeye na kujishughilha katika kumtii ye yaani khalifa.

Bwana wetu mpendwa Mtume mtukufu s.a.w. alituelezea umuhimmu wa kujiunga na Imam wa zama akisema ;

ان رئیت یومئذ خلیفۃ اللہ فی الارض فالزمہ ان نھک جسمک و اخذ مالک

kama ukimwona Khalifa wa Allah ardhini, basi ushikamane naye hata kama (kwa sababu ya kujiunga naye) mwili wako ukaadhibiwa vikali na hata kama ukanyang'anywa mali yako. (Musnad Ahmad)

Safari moja Hazrat Mirza Bashiruddin Mahmood, Khalifatul Masihi wa pili alitufafanulia hivi kwamba:

"Yupo mtu kwa ajili yenu, anayejisikia maumivu yenu kuwa maumivu yake, anayewapendeni, anayezichukua shida zenu kuwa shida zake, anayejaali taabu zenu kama za kwake, anayewaombeni dua kwa Mungu; lakini (wapinzani) hawana mtu yeyote kama huyu, mtu huyu analia mbele ya Mungu kwa ajili yenu na hakuna yeyote kwa ajili yao. (Anwar ul ulum j.2.uk.156)

Safari moja, Khalifa wetu wa tano (atba) alisema akieleza hali yake halisi kwamba: "

"Khalifa wa zama anakuwa na uhusiano wa dhati na kila mwahmadiyya wa kila taifa, na wa kila kabila, wa dunia nzima. Anapata barua zao zielezazo mambo binafsi. Huu ndio ukhalifa tu unaojali shida ya kila mwahmadiyya wa dunia. Khalifa anawaombea dua. Ni nani miongoni mwa viongozi wa dunia hii ambaye huwaombea wagonjwa. Ni nani mwingine anayesikia uchungu juu ya changamoto za ndoa za mabinti wa jumuiya yake na kuwaombea dua, …… Wanajamati ndio wenye bahati ambao khalifa wao huwaombea dua, anajali afya yao, elimu yao, na mambo yao ya ndoa, kwa ufupi, hakuna tatizo lolote la waahmadiyya duniani ila Khalifa analijua na kujitahidi kwa ajili ya kuliondoa na kuwaombea dua kwa Mwenyezi Mungu. Makhalifa waliokuwa kabla yangu pia walikuwa wanafanya hivyo na mimi ninafanya hivyo. Hakuna nchi duniani ila ninafika huku kwa mawazo yangu kabla ya

Ukurasa 08

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi Ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

Kuelekea Ijtimaa ya Kitaifa Lajna Imaillah

UK. 03






Ukhalifa- Chanzo cha Baraka Zote



Na. Sheikh Karim Uddin Shams, Dodoma.

Mwenyezi Mungu Alimuumba binadamu kuwa kiumbe kilicho bora zaidi na kumuumba kwa rasimu iliyo bora zaidi miongoni mwa rasimu za uumbaji wake. Hii ndiyo kawaida yake Mungu Mwenye Enzi iliyoenea katika dunia hii kwamba huwatuma manabii kwa ajili ya kuwaongoza wanadamu wakati wa giza nene na totoro. Mbegu ya uongozi wa kiungu hupandwa na manabii hawa na mbegu hii huota na kukuwa wakati wao. Kwa hakika, kuja kwa manabii na mitume hawa huwa dhihirisho la kudra ya kwanza ya Mwenyezi Mungu nao huitwa makhalifa wa Allah Mtukufu Subahanahu wataala. Manabii wamepewa jina la Khalifa ndani ya Kurani Tukufu kama Hazrat Adam a.s.na Hazrat Daud a.s. kwa kweli cheo hiki ni cha kila nabii wa Allah Mtukufu.



Mwenyezi Mungu mwenye kujua hekima nyingi hata za siri kabisa, Alianzisha kanuni Yake hivi duniani kwamba wakati unapofika wa kuondoka na kufariki kwa nabii basi kwa ajili ya kukamilisha kazi zake ambazo bado hazijakamilika vizuri na ili kuendeleza mbele kazi zake pamoja na kuwalea vizuri wanajumuiyya wake na kuwapa maendeleo na mafanikio makubwa zaidi hadi kuyafikisha kileleni, Anaonesha muujiza wa kudra yake ya pili na kuudhihirisha kwa sura ya Ukhalifa. Waaminio wanamchagua mmoja wao kwa uongozi wa Allah Mtukufu na uchaguzi huu unakuwa uchaguzi wa Mwenyezi Mungu kwa hakika; na taji la ukhalifa huvalishwa kwa mja huyu kwa idhini ya Mwenyezi na huyu naye katika istilahi ya dini anaitwa *Khalifa tur Rasool* (khalifa wa Nabii). Kiongozi huyu wa kiroho wa Jumuiyya ya waaminio, anatekeleza majukumu yake na wajibu wake huku akisukuma na kusogeza

UK. 11

A GIFT TO CHRISTIANS

BY

SHEIKH MUZAFFAR AHMAD DURRANI

This is a book written in Kiswahili Language which contains many the controversial topics about Christianity, for example:

God is One
Jesus in the Holy Quran
Muhammad s.a.w. in the Bible
Jesus a.s. in Not a God
Jesus a.s. did not Die on the Cross
Second coming of Jesus a.s.
Some Contradictions in the Bible
Removed and added verses in the Bible
... and many other interesting topics.

ISBN 9987- 8932- 5-2

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

ZAWADI KWA WAKRISTO

MUNGU WA KWELI NI MMOJA TU

MUHAMMAD S.A.W. KATIKA BIBLIA

YESU A.S. KATIKA QUR'AN

SHEIKH MUZAFFAR AHMAD DURRANI

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 1,550/=.

Je, Wajua?

Je wajua kuwa ili uone kitu, basi mwanga unaotoka katika kile kitu unatakiwa uwe umefika machoni kwako. Mwanga wa jua unatumia dakika nane kufika duniani. Mwanga wa nyota unachukua miaka milioni kadhaa kufika duniani. Hivyo uonapo nyota, fahamu kwamba unachokiona hasa ni mwanga uliotoka katika nyota miaka milioni iliyopita, na unafika katika macho yako muda huo unaoangalia. Unachokiona sio sasa, unaona historia. Wanasayansi wanatumia historia hiyo kujua dunia iliumbwaje.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com